TANGAZO LA SERIKALI NA. 1045 la tarehe 13/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

---

# NOTISI

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MABADILIKO YA ENEO LA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA NYANTAKARA YA MWAKA 2024

KWA KUWA, Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara lilitangazwa chini ya kifungu cha 25 cha Sheria ya Misitu, Na. 30 ya Mwaka 1957 kuwa Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara;

KWA KUWA, Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kufanya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara;

NA KWAKUWA, Waziri kwa kuzingatia Sheria ya Misitu Sura ya 323 ambayo, pamoja na masharti mengine inamtaka, anapokusudia kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa, kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

HIVYO BASI, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

2. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara.

Madhumuni ya mabadiliko

3. Madhumuni ya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara ni-

(a) kujumuisha eneo lote la ardhi ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa Nyantakara baada ya eneo hilo kupimwa upya kwa kutumia njia za upimaji na uchoraji ramani za kisasa; na
(b) kuhifadhi baioanuwai, vyanzo vya maji ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

4.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakaraambalo linapendekezwa kubadilishwa.

Uwasilishaji wa pingamizi

5. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Nyantakara, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

---

JEDWALI

---


*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA BIHARAMULO
MSITU WA HIFADHI WA NYANTAKARA

Makadirio ya eneo: Hekta 49,280 au Kilometa za Mraba 492.28

Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Nyantakara linalopatikana Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera kama lilivyochorwa katika




SCHEDULE

| BEACON NO. | TRUE BEARING | DISTANCE IN METRES | COORDINATES EASTINGS | NORTHINGS |
|---|---|---|---|---|
| FD-1 | | | 305949 | 9662964 |
| | 132°13' | 5154 | | |
| FD-2 | | | 309765 | 9659500 |
| | 281°16' | 1615 | | |
| FD-3 | | | 308181 | 9659816 |
| | 149°43' | 1964 | | |
| FD-4 | | | 309171 | 9658120 |
| | 155°31' | 11060 | | |
| FD-5 | | | 313753 | 9648054 |
| | 121°54' | 3334 | | |
| FD-6 | | | 316583 | 9646292 |
| | 143°52' | 5628 | | |
| FD-7 | | | 319901 | 9641746 |
| | 224°11' | 612 | | |
| FD-7a | | | 319474.5 | 9641307.274 |
| | 191°42' | 904 | | |
| FD-7b | | | 319291.2 | 9640422.364 |
| | 225°18' | 2024 | | |
| FD-7c | | | 317852 | 9638998.728 |
| | 209°44' | 831 | | |
| FD-7d | | | 317439.7 | 9638277.186 |
| | 184°31' | 938 | | |
| FD-7e | | | 317365.8 | 9637341.709 |
| | 145°27' | 144 | | |
| FD-7f | | | 317447.5 | 9637223.073 |
| | 185°18' | 2840 | | |
| FD-7g | | | 317184.9 | 9634395.249 |
| | 148°8' | 1113 | | |
| FD-7h | | | 317772.2 | 9633450.048 |
| | 129°26' | 1399 | | |
| FD-7i | | | 318852.6 | 9632561.248 |
| | 111°33' | 503 | | |
| FD-7j | | | 319320.4 | 9632376.486 |
| | 238°43' | 6198 | | |
| FD-8 | | | 314023 | 9629159 |
| | 149°6' | 2684 | | |
| FD-9 | | | 315401 | 9626856 |
| | 266°3' | 7493 | | |
| FD-10 | | | 307926 | 9626340 |
| | 336°37' | 829 | | |
| FD-10a | | | 307597 | 9627101 |
| | 0°49' | 1108 | | |
| FD-10b | | | 307613 | 9628209 |
| | 347°44' | 2884 | | |
| FD-10c | | | 307001 | 9631027 |
| | 356°6' | 1976 | | |
| FD-10d | | | 306867 | 9632998 |
| | 340°9' | 283 | | |
| FD-10e | | | 306771 | 9633264 |
| | 316°30' | 350 | | |
| FD-10f | | | 306530 | 9633518 |
| | 293°20' | 3737 | | |
| FD-10g | | | 303099 | 9634999 |
| | 275°17' | 758 | | |
| FD-10h | | | 302344 | 9635069 |
| | 322°44' | 824 | | |
| FD-10i | | | 301845 | 9635725 |
| | 347°36' | 489 | | |
| FD-10j | | | 301740 | 9636203 |
| | 312°2' | 1538 | | |
| FD-10k | | | 300598 | 9637233 |
| | 296°12' | 990 | | |
| FD-10l | | | 299710 | 9637670 |
| | 292°53' | 962 | | |
| FD-10m | | | 298824 | 9638044 |
| | 280°44' | 1556 | | |
| FD-10n | | | 297295 | 9638334 |
| | Curvilinear (Mtundu river) | 36538 | | |
| FD-1 | | | 305949 | 9662964 |

Ramani Na. Jb 3183 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:

Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA
*Waziri wa Maliasili na Utalii*